

Kiamu na Usomi wa Kale wa Waswahili

Dennis Simiyu

Chuo Kikuu cha Mt. Lawrence, Canton, New
York

simiyumunyole@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza nafasi ya lahaja ya Kiamu kama lugha ya usomi baina ya Waswahili katika Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa wageni na kusanifishwa kwa Kiswahili. Utafiti huu ni wa kimaktaba ambapo data za msingi zimepatikana kwa mbinu ya kimaktaba. Uchambuzi wa data umeongozwa na nadharia ya Daiglosia. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa lahaja ya Kiamu ndiyo ilipewa hadhi ya juu ya kutumika kama lugha ya usomi wa Waswahili katika jamii za Afrika Mashariki. Pia, inahitimisha kuwa lahaja ya Kiamu ni lahaja muhimu katika historia na maendeleo ya jamii ya Waswahili na matumizi yake katika nyanja za sarufi, fasihi na uandishi zilitumiwa kuipa sifa ya kitaaluma kazi inayohusika. Makala hii inapendekeza kuwa Kiamu kutumika katika usomi wa kale wa jamii ya Waswahili kabla ya usanifishaji wa Kiswahili haina maana kwamba lahaja ya Kiamu ilikuwa bora kuliko lahaja zingine bali ilipewa tu hadhi ya kutumika katika shughuli za usomi. Uchunguzi zaidi kuhusu matumizi ya Kiamu katika visiwa vya Komoro, Unguja na sehemu za Kongo ni muhimu.

Maneno Msingi: Lugha ya Usomi, Kiamu, Waswahili, Lahaja na Daiglosia.

Utangulizi

Makala hii imechunguza nafasi ya lahaja ya Kiamu kama lugha ya usomi baina ya Waswahili katika Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa wageni na kusanifishwa kwa Kiswahili. Watafiti wa awali wa lahaja za Waswahili wamebainisha kwamba kuna zaidi ya lahaja 15 za Kiswahili kama inavyoelezwa na Stigand (1915), Palome (1967), Chiragdin (1977) na Karanja (2012). Wengine ni Hennesbeuch (1996), Nabhany (1995) na Khalid (1977) wanaotaja lahaja 20 za Kiswahili bila kuitaja lahaja ya Kiunguja. Lahaja ya Kiunguja ndiyo iliyochaguliwa kama msingi wa usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, Khalid alitaja lahaja za Kisokotra na Kimafia ambazo hazikuwa zimetajwa na wataalamu wengine.

MAKALA HALISI

HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 09 Julai 2021

Kurekebishwa: 12 Sept. 2021

Kukubaliwa: 18 Oktoba 2021

Kuchapishwa: 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 20 – 28.

NUKUU: Simiyu, D. (2021). Kiamu na Usomi wa Kale wa Waswahili. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, 7(2), 20 – 28.

Lahaja nyingi za Kiswahili zimepewa majina kulingana na sehemu ya kijiografia ambako zinazungumzwa. Kwa mfano, Kiamu huzungumzwa Lamu, Kimvita huzungumzwa Mvita na Kipate huzungumzwa katika Kisiwa cha Pate. Lahaja za Kiswahili huzungumzwa kutoka Kusini mwa Somalia Kaskazini mwa Kisiwa cha Komoro Kusini. Lahaja hizi huzungumzwa pia nchini Kenya, Tanzania, visiwa vya Zanzibar na Komoro. Utafiti huu umechunguza lugha ya Kiamu kama lugha iliyotumiwa na Waswahili katika taaluma, hasa fasihi, elimu na mawasiliano katika shughuli nyingine za kijamii. Ufafanuzi huu hauna maana kwamba lahaja zingine hazikutumika katika baadhi ya shughuli. Kwa mfano, baadhi ya jamii za Waswahili, hasa kutoka Lamu walitumia lahaja ya Kingozi katika kuendeleza shughuli za baraza na hata utunzi wa mashairi. Hali hii pekee haiwezi kuipa lugha hadhi ya kuwa ya usomi.

Lugha ya Kiswahili sanifu ilibuniwa baada ya Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (*EastAfrica Inter-territorial Swahili Language Committee*) kukamilisha shughuli ya usanifishaji. Harakati ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ilianzishwa na Gavana wa Tanganyika mwaka wa 1925 baada ya ripoti ya tume ya Phelp-Stokes kuchapishwa. Wasanifishaji walilenga kutatua mgogoro na changamoto zilizotokana na mawasiliano katika biashara, dini, utawala na elimu. Kuna wale waliopendelea Kiunguja, Kimvita na Kiamu. Licha ya lahaja ya Kimvita na Kiamu zilisemekana kuwa na historia ndefu na kufanyiwa utafiti mwingi, Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliichagua lahaja ya Kiunguja kutumiwa kama msingi wa usanifishaji wa Kiswahili. Mbaabu (2007) anaeleza:

Kiunguja hakikuwa kimestawi sana kwa upande wa fasihi andishi kabla ya kuja kwa Wamisheni na kuchapishwa kwa vitabu vya kina Madan na Steer. Huu ulikuwa upungufu mkubwa, tukilinganisha Kiamu na Kimvita, lahaja zilizokuwa zenye miswada mingi ya ushairi, kidini na kifasihi (Mbaabu, 2007:13).

Kutokana na maoni haya hapo juu, inawezekana Kiunguja kilichaguliwa kwa sababu ya ushawishi wa kibiashara na nguvu za kiutawala. Kabla ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili, Waswahili walikuwa na lugha ya usomi. Lugha hii ilikuwa ni lugha ya Kiamu. Kulingana na Nurse na Thomas (1993) huenda lahaja tofauti ilitumika katika vijiji vya Ozi karibu na ukingo wa mto Tana na huenda vilipotea na nafasi yake kuchukuliwa na Kiamu. Jambo hili linamaanisha Kiamu kilikuwa kimeenea sana. Bakari (1985), Nurse (1982b), Prins (1967) na Sacleux (1909) wanaafikiana na maelezo haya kwa kusema kuwa, kihistoria Lamu ilikuwa na lahaja nyingi zaidi kuliko leo ambazo zilimezwa baadaye na Kiamu.

Knappert (1967, 1977 na 1979) anaeleza kwamba utenzi wa Al-Inkishafi uliandikwa kwa lahaja ya Kiamu. Khalid (1977) anaeleza kuhusu umaarufu wa lahaja ya Kiamu ambayo ilitumika na kuvuka mipaka kisiwa cha Komora na baadhi ya sehemu za

Pwani ya Tanzania. Abdulaziz (1979) anafafanua uhusiano wa lugha ya Kiamu na Kimvita katika mashairi ya Muyaka. Abdulazizi anaeleza sababu zilizosababisha watunzi wa Kimvita kutumia Kiamu katika utunzi. Kwa upande mwingine, Bakari (1985) alibainisha matumizi ya muundo wa fonolojia na mofolojia ya Kiamu katika mashairi na maandishi ya Kimvita na lahaja nyingine za Kiswahili. Pia, Hitchens na Mlamala (1939) wanaeleza jinsi Kiamu kilivyoathiri utunzi wa mashairi ya Muyaka. Nurse na Thomas (1993) lahaja za Kiswahili na tarakimu ya wazungumzaji.

Mbaabu (2007) mbali na kuzungumzia masuala mengi kuhusu lugha ya Kiswahili na usanifishaji, anaeleza mjadala uliyokuwapo baina ya wataalam kama vile Medan, Steere na Askofu Krapf kuhusu lahaja ambayo ilistahili kuchaguliwa kama kielelezo cha usanifishaji wa Kiswahili. Lahaja za Kiamu, Kimvita na Kiunguja zilipendekezwa. Pia, anaeleza mambo yaliyosababisha Kiunguja kuchaguliwa. Mthubi (2015), Mazrui (2007) na Kea (2006) wameeleza nafasi ya Kiamu kama lugha ya usomi katika jamii za Waswahili. Makala hii imechunguza Kiamu kama lugha ya kale ya usomi katika jamii za Waswahili.

Mbinu na Nadharia ya Utafiti

Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala hii umeongozwa na nadharia ya Daiglosia. Nadharia ya Daiglosia iliyoasisiwa na Ferguson mwaka 1959 (Mmarekani). Ferguson anaeleza kuwa katika mazingira yenye lugha zaidi ya moja, lugha ya juu hutumika katika shughuli maalum na watu (Fishman, 1967). Lugha ya juu au chini inaweza kutumiwa na wazungumzaji wa lugha zaidi ya moja wanaotoka katika mazingira tofauti. Pia, wazungumzaji wa lugha tofauti na katika katika mazingira tofauti wanaweza kusikilizana na kuifanya lugha moja kuwa ya juu katika mawasiliano yao. Katika makala hii nadharia hii imetumika kueleza sababu zilizosababisha lahaja ya Kiamu katika mawasiliano yao ya kirasmi na kitaaluma. Utafiti huu ni wa kimaktaba. Data za msingi zimepatikana kwa mbinu ya kimaktaba. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika ili kufanikisha lengo mahsusi la uchunguzi.

Lahaja ya Kiamu Katika Jamii ya Waswahili

Chimbuko la Waswahili na historia yao ya usomi lazima tuzingatie ukweli kuwa usTaarabuu wa Waswahili hupatikana katika sanaa yao kama vile katika tendi, hekaya, habari na masimulizi. Lugha ya usomi katika jamii yoyote hupatikana katika sanaa na fasihi ya jamii hiyo (Rollins, 1983). Makala hii imezingatia ithibati mahsusi ili kuthibitisha kuwa lugha ya Kiamu ilitumika na Waswahili kama lugha ya usomi kabla ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii za Pwani ya Afrika Mashariki. Miongoni mwa mambo yanayothibitisha kuwa Kiamu ilitumika kama lugha ya usomi kabla ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili yameelezwa katika sehemu hii.

Fasihi na Tenzi za Waswahili

Kitovu cha lugha na fasihi ya Waswahili ni Lamu (Polome, 1967). Jambo hili lina maana kwamba fasihi ya Waswahili ina usuli wake katika lugha ya Kiamu. Kiamu

ndiyo ilikuwa lugha ya kale ya usomi ya Waswahili. Kwa mfano, mtu akitaka kunukuu mashairi ya Pwani ya Kenya, hasa ya Waswahili wa kale akiwa Chuo Kikuu kule Uingereza ama bara lolote lile, atatumia Kiamu. Jambo hili linajitokeza hivi kwa sababu hata watunzi wa mashairi wanaozungumza lahaja ya Kimvita walitunga mashairi wakati huo kwa kutumia lahaja ya Kiamu. Hata sasa wanatumia lahaja ya Kiamu na kuongezea maneno ya lahaja ya Kimvita ili yaweze kuimbika kwa sababu utunzi wao wa awali ulijikita katika lugha ya usomi ambayo ni Kiamu. Maelezo haya yanadhibitishwa na maelezo ya Fishman (1967) kuwa kila wakati mzungumzaji wa lugha zaidi ya mbili anapotaka kuwasilisha ujumbe fulani, hulazimika kutumia lugha yenye hadhi ya juu.

Tenzi za Kale

Mbaabu (2007) anathibitisha kuwa mashairi mengi ya jadi yalitungwa kwa kutumia lahaja ya Kiamu. Umarufu wa Kiamu uliwachochea Wazungu kama vile Alice Wener kupendekeza lahaja ya Kiamu ichaguliwe kuwa lahaja ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki karne ya ishirini. Utenzi wa *Al-Inkishafi* uliandikwa miaka 1000 baada ya Kristo. Dhamira ya mtunzi wa utenzi huu ilichimbuka kutokana na mazingira ya himaya ya Pate na masalia yake ambapo ameeleza maisha ya anasa ya wafalme wa Pate pamoja na anguko la Pate. Nurse na Thomas wanaeleza kuwa Pate ilikuwa na lahaja yake tofauti na Kiamu, mtunzi anatumia Kiamu zaidi kuliko lahaja nyingine kama vile Kingozi na Kiarabu. Pia, mtunzi wa *Al Inkishafi* alitumia lahaja ya Kiamu katika utunzi wake (Knappert, 1967). Baadhi ya maneno ya Kiamu aliyotumia ni kama Nduye (ub.2), Maina (ub. 4), kuisa (ub. 10), Zanda (ub. 22), zango (ub.39), huvunda (ub.77), mai (ub. 53). Mtunzi alitumia Kiamu kwa msingi kuwa ilikuwa lugha ya usomi.

Katika utendi wa *Fumo Liyongo* uliotungwa na Bwana Muhamad bin Abubakar bin Omar al-Bakry (Muhamad Kijumwa) mwaka (1913) ambaye aliipata hadithi hii kutokana na mapokezi simulizi ya Waswahili na kisha kuisimulia upya katika umbo la Utendi (Mulokozi, 1999). Utendi huu unamrejelea Liyongo ambaye baadhi ya wataalam wanasema aliishi Ozi na wengine wanasema Pate. Mtunzi ametumia Kiamu na maneno machache ya Kingozi na Kiarabu. Baadhi ya maneno ya Kiamu ni kama ina (ub.1), watakaokuya (ub.1), mkoyo (ub. 14), Ndime (ub.37), zigongo (ub. 86), mayiwe (ub. 282) na maneno mengine mengi ya Kiamu. Hii ina maana kuwa Kiamu kilikuwa kimeenea sana na kilikuwa kinatumika kote Uswahilini.

Watunzi wa Kimvita na uhusiano wao na lugha ya Kiamu ni kwamba mashairi ya Muyaka ya kati ya 1800 na 1840 yameandikwa kwa lahaja ya Kimvita. Kimvita ni lahaja iliyokuwa ikitumika Mombasa alikoishi Muyaka. Mashairi haya yana athari ya lahaja za Kiamu. Hichens (1939) anaafiki maelezo haya kwa kueleza kuwa lugha ambayo ilitumiwa na Muyaka inasukumwa mbele na Kiamu kilichoandikwa. Anasema hivi:

Washairi walio mashuhuri Mombasa, Muyaka akiwa mmoja wao, walitunga kwa lugha ambayo ina ukuruba na matumizi ya Kimvita, lakini ina mwelekeo wa Kiamu kama kielelezo chake (Abdulaziz 1979: 69).

Haya maelezo yana ukuruba na jinsi nadharia ya daiglosia inavyoeleza kuwa katika mazingira yenye kuwa lahaja zaidi ya moja, lahaja moja huteuliwa ili kutumiwa kama lahaja ya juu. Muyaka na watunzi wengine wa fasihi ambao sio wazungumzaji wa Kiamu walijaribu iwezekanavyo kazi zao kuwa na mwelekeo wa Kiamu ili ziweze kukubalika na jamii ya wasomi wa Waswahili.

Sarufi ya Kiamu

Unapoyasoma mashairi ya Muyaka kuna msamiati na viarifa vya nyakati vinavyolingana na matumizi yanayopatikana katika lahaja ya Kiamu. Haya yanatokea kwa sababu Kiamu ndicho kilikuwa kitovu cha fasihi ya Waswahili. Kila mshairi aliwajibika kutumia sifa fulani za kiisimu za lahaja ya Kiamu ili kuongeza haiba katika kazi yao. Tukiangalia shairi lake la *Mpiga Mayi*:

Mpiga *mayi* mak'wanda ni kutaka kuyatua,
Ndilo sumbuko la *kwanda* kupenda *asiyoyua*,
Laiti mwele *konda* tamuye ha tambua,
Nguvu zangu na takuwa zinishizile nyangwani (Abdulaziz 1979: 322).

Katika mfano huu, matumizi ya Kimvita na Kiamu yanajitokeza sambamba. Mtunzi ametumia neno *Mayi*, *kwanda*, *asiyoyua* na *konda*. Maneno haya yanapatikana katika lahaja ya Kiamu na pia hutumika katika Kimvita. Pia, Muyaka ametumia sana kiambishi cha zamani {-le} ambacho pia kimetumika sana na watunzi wa kale katika Kiamu. Kwa mfano, katika shairi lake *Uovu ni Vule*:

Ouvuo ni uule, kula wakati k'ongea,
Ukele kwa nia mbile, mbi iliyotopea,
Mwandani unitoshile, feeli zako ni mbaya,
Mzigo umenemea, tautua nipumue (Abdulaziz, 1979: 222).

Mfano huu unatuonesha vile Muyaka ametumia maneno kama vile *uule*, *mbile*, *ukele*, *unitoshile* na *umenemea* ambayo ni ya muundo ambao washairi wa kale walitunga kwa Kiamu. Kiambishi hiki kimetumika sana kimofolojia kama kiishio cha vitenzi katika mashairi yaliyoandikwa zamani kwa Kiamu ili kuonesha kitendo kilitendeka na kilikamilika. Abdulaziz (1979) ana maoni tofauti kuhusu namna Muyaka alivyotumia msamiati wake. Alichunguza msamiati uliotumiwa katika mashairi ya Muyaka na kubainisha kuwa Muyaka alikiuka kimsamiati kwa kutumia maneno ya Kiamu badala ya Kimvita. Alifanya hivyo kufuata mtindo wa lahaja ambayo ilikuwa ya usomi Uswahilini.

Pia, utenzi wa *Swifa wa Nguvumali* ambao ni utenzi wa Kusini unaosimulia kisa cha ajabu eneo la Kilwa kuhusiana na jinsi mauaji ya mwanamke mmoja yalivyosababishwa na wachawi na baadaye waligunduliwa na mganga maarufu

ajulikanaye kama Nguvumali. Mtunzi wa utenzi huu ametumia lahaja ya Kimrima ambayo ni ya Kusini. Hata hivyo, mtunzi ametumia lahaja ya Kaskazini ya Kiamu ambapo ametumia sauti [Y] badala ya [J] ya Kiswahili sanifu. Ametumia maneno kama vile ‘moya’ badala ya ‘moja’ ‘wanayua’ badala ya ‘wanajua’. Jinsi tunavyoona, maneno haya ni ya Kiamu ambayo yametumika kwa kuwa ndiyo ilikuwa lugha ya usomi kwa wakati huo. Katika utenzi wa *Maulidi ya Nuni* mwandishi umetumia Kiamu. Katika ubeti wa nne (4), mtunzi anasema kwamba ametoa tafsiri ya utenzi kwa Kiamu ili watu wote wausome waelewe.

Ubeti huu unaonesha wazi kwamba mtunzi hakutumia lahaja ya Kiamu kwa nia nyinngine ila kwa sababu Kiamu ilikuwa ni kituo cha kiusomi kabla ya karne ya Ishirini. Utenzi wa *Maulidi ya Nuni* ulitungwa na Sharifu Mansabu’ Abdul Rahmani al Husaini mwaka wa 1891. Kwa mujibu wa mtunzi wake, utenzi huu ulitungwa sehemu ya Pate ulikuwa na ni tafsiri ya *Maulidi ya Barzanji* (Knappert 1971). Fishman (1967) anaeleza kwamba katika mazingira daiglosia mzungumzaji wa lugha au lahaja ya chini hulazimika kutumia lahaja ya juu ambayo ina hadhi ili ujumbe wake uweze kuwafikia watu wengi. Watunzi wa mashairi ya *Muyaka*, *Utenzi wa Maulidi ya Nuni* na *Swifa ya Nguvumali* walikuwa wanajaribu kutumia lahaja yenye hadhi ya usomi ambayo ni Kiamu.

Sura za kimuundo za mashairi ya Waswahili ziko sawa Uswahilini kote, yaani zimeiga muundo wa tenzi za kwanza ambazo ziliandikwa kwa Kiamu. Mashairi yote ya Waswahili yalikuwa na utangulizi uliotoa sala kwa Mungu au kuitisha vifaa vya kuandika au kuwataja wale anaotaka wapate ujumbe wake. Pili, mtunzi alitoa lengo la kutunga lililofuatwa na masimulizi marefu ya visa ambavyo vilibeba maudhui. Watunzi walimaliza kwa sala kwa Mwenyezi Mungu. Aghalabu, Mtume na swahiba wake walitajwa pamoja na nasaba ya mtunzi. Pia, aliomba radhi ikiwa amekosea yeyote ama ikiwa kuna kasoro katika utenzi wake.

Mbali na sifa hizi kuwemo katika utenzi wa *Al-Inkishafi*, *Mwana Kupona*, utenzi wa *Fumo Liyongo*, *Takhmisa ya Liyongo* pia imejitokeza katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na mashairi ya *Muyaka*. Shairi la *Muyaka* la “*Ukiwa Wako*” (uk. 209) ubeti wa sita anakamilisha kwa kusema kuwa amefika tamati na anaomba msamaha ikiwa amechukiza katika utenzi wake. Katika shairi la “*Ugosi*” (uk. 210) anaanza kwa kutuma karatasi ya Kituruki kwa rafikiye. Anaeleza karatasi kuwa imrudishie jibu kwani hataki ifanye kosa lolote. Katika aya ya mwisho ya shairi hili, mtunzi anaeleza kuwa anakamilisha kwa kuwazingatia werevu wa vanga. Mashairi mengine ya *Muyaka* yenye sifa hizi ni “*Mangi Mafilia Ndani*” na “*Ukiwa Wako*. Katika utenzi wa *Swifa wa Nguvumali*, mtunzi alianza kwa kumtukuza Mungu na kumaliza kwa shukrani kwa Mwenyezi mungu. Ubeti wa kwanza unianza kwa maneno haya:

Bismilahi naanza,
Juna la mola wa enza,
Muhammad mpendeza,

Kwa mola wetu jalia.

Mifano hii ya tungo za kale zaidi katika pwani ambazo zimetungwa na kuandikwa kwa lugha ya kipekee ambayo ni Kiamu ina maana kwamba lugha ya usomi baina ya lahaja mbali mbali za pwani ilikuwa Kiamu.

Tarikhi za Kale na Fasihi Simulizi

Kulingana na Khalid, fasihi ya Zanj (Jina lilotumiwa na Al-Masud katika safari yake ya Afrika Mashariki akirejelea wakazi wa sehemu hii kuanzia Sofala hadi Mogadishu). Jina hili lina maana ya watu weusi ambao Khalid anarejelea kama Waswahili ilichipuka katika Kisiwa cha Amu Fungu visiwa karibu na Kusini. Anaendelea kueleza kuwa hata fasihi ya wazungumzaji wa Kipemba na Kitanga waliathiriwa na wakaazi wa Kisiwa cha Mombasa ambao walikuwa wameshapata athari kutoka lahaja ya Kiamu kule Lamu. Kutokana na maelezo ya Khalid, tunaweza kueleza kuwa matumizi ya lahaja ya Kiamu kama lugha ya usomi kabla ya Wakoloni na Waarabu kuingia Afrika Mashariki ilikuwa kigezo muhimu katika usambazaji wa fasihi na lahaja ya Kiamu.

Masimulizi ya Halldin

Hatimaye, makala hii hayawezi kukamilika kabla mwanasayansi mmoja, Swen Halldin alifanya utafiti Pwani ya Kenya. Alipokuwa katika harakati ya kufanya utafiti wake, alipendezwa sana na fasihi ya Waswahili. Jambo hili lilimfanya achukue nusu ya mwaka ambayo ilikuwa sehemu ya utafiti wake kufanya utafiti kuhusu wenyeji wa Pwani. Halldin alikuwa na maelezo yafuatayo kuhusu lugha iliyotumiwa na Waswahili kama ya usomi:

Fasihi ya Waswahili imejengeka katika lahaja ya Kiamu. Kwa hivyo, sehemu yao ya lugha ya usomi ni Kiamu, bali sio Kimvita kama wengine wanavyoeleza (Khalid, 1977:78).

Maelezo haya yanatokana na ukweli kuwa Kiamu kina utajiri mkubwa katika miundo ya sarufi, hasa katika misamiati ya kitamaduni kuliko lahaja nyingine za Kiswahili kama vile Kimvita. Kutokana na utafiti wake Halldin, mwalimu wa Kiamu atapata wakati mgumu kufunza Kimvita kuliko mwalimu wa Kimvita kufunzia Kiamu kwa sababu Kiamu ni sehemu ya kila Mswahili. Tofauti hii inajitokeza kwa sababu Kiamu kilikuwa kinajulikana karibu na kila mtu na sarufi yake ilikuwa inapatikana katika lahaja nyingi za Kiswahili. Ingawa Kiamu ni rahisi kwa Waswahili, mtu kutoka bara ataelewa Kimvita kuliko Kiamu.

Halldin alikutana na mkuu wa kitengo cha uhamiaji kule visiwa vya Komora. Halldin alipomuuliza ikiwa lugha hiyo yake ya Kingazija ina utajiri kuliko Kiswahili cha Tanzania, mkuu wa idara alikubali kuwa ni ukweli lugha yake ina utajiri kuliko Kiswahili cha Tanzania. Mkuu huyu alipoulizwa na Halldin ikiwa lugha yake ina utajiri kuliko Kiamu, mkuu huyo wa idara alikanusha na kusema kuwa Kiamu kina utajiri mkubwa kuliko lugha yake. Aliongezea kuwa ana maandishi yaliyoandikwa

miaka mia na zaidi ambayo yanakaribiana na Kiamu cha sasa. Kutokana na maelezo haya ya huyu mwanasayansi, ni wazi kuwa lugha ya usomi wa kale wa Waswahili ilikuwa Kiamu.

Hitimisho

Lugha ya usomi katika jamii yoyote hupatikana katika sanaa na fasihi ya jamii hiyo (Rollins, 1983). Kitovu cha lugha na fasihi ya Waswahili ni Lamu (Polome, 1967). Fasihi ya Waswahili ina usuli wake katika lugha ya Kiamu basi lugha hii ndiyo ilikuwa lugha ya kale ya usomi ya Waswahili. Matumizi ya sarufi ya lahaja ya Kiamu katika fasihi na maandishi ya lahaja nyingine kama vile Kimvita hayakuwa ya kubahatisha, bali maandishi walijaribu kutumia lahaja ya juu ambayo ilikuwa Kiamu ili kazi yao ionekane kuwa ya kitaaluma. Matumizi ya Kiamu katika shughuli za usomi yanaonyesha jinsi Waswahili walikuwa wamepanga sera yao ya lugha kabla ya ujeo wa wakoloni. Mbali na kuendelea kufanyia uchunguzi na uhifadhi wa lahaja ya Kiamu, ni vyema pia lahaja zingine za Waswahili zifanyiwe utafiti ili kuimarisha na kufahamu utamaduni na lahaja za Waswahili. Pia, hatuna budi kuchunguza zaidi matumizi ya Kiamu katika Visiwa vya Komoro, Unguja na hata Kongo.

Marejeleo

- Abdulaziz, M. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Bakari, M. (1985). *The Morphology of the Kenyan Swahili Dialects*. Berlin: Dietrich Reimer.
- Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.
- Ferguson, C. (1959). Diglossia. *Word* 15. 325-340.
- Fishman, J. A. (1967). Bilingualism with and Without Diglossia; Diglossia With and Without ingualism. *Journal of social Issues*, 23. 29-38.
- Hinnesbusch, T. (1996) 'What kind of language is Swahili?' *AAP* 47, 73-95.
- Hitchens, W. (1972). *Al- Inkishafi: The Sauls Awakening*. Ed. 1939 Sayyid bin Abdalla bin Ali bin Nassir. London: The Sheldon Press.
- Kea, P. (2006). Usemezo katika Nyimbo za Taarabuu. *Tasnifu ya Umahiri*, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Khalid, A. (1977). *The Liberation of Swahili from European Appropriation*. Nairobi. East African Bureau.
- Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry*. Laiden: Brill.
- Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heinemann.
- Mazrui, A. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language and Identity*. Athens: Ohio Press.

- Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mbaabu, I. (2007). *Historia na Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar Es Salaam; Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mlamali, M. (1980). *Ikisiri*. Nairobi: Longman.
- Mthubi, F. (2015). Mikakati na Mbinu za Usimilishwaji katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Nurse, D. (1982b). *The Swahili Dialects of Somalia and the Northern Kenya Coast*. Katika M-F. Rombi, 73-146.
- Nurse, D., na Thomas, J. (1993). *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. London: University of California Press.
- Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center for Applied Linguistics.
- Prins, J. (1967). *The Swahili Speaking People of Zanzibar, and the East African Coast (Arabs Shirazi and Swahili)*. London; International African Institute.
- Rollins, J. D. (1983). *A History of Swahili Prose*. Leiden: E. J. Brill.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es salaam University Press.
- Stigand, C. H. (1915). *A Grammar of Dialects Changes in the Kiswahili Language*. London: Cambridge University Press.
- Sacleux, C. (1909). *Grammaire des Dialectes Swahilis*. Paris: Procure des PP. Du Saint-Espirit.